# JARIDA la Mamlaka ya Serikali Mtandao

Toleo Na. 3 Januari - Machi 2023




"Uadilifu na Ubunifu kwa Utoaji Huduma Bora kwa Umma"

*Karibu tujenge Serikali Kidijitali*

ega_tanzania   ega online tv

# KUTOKA KWA MKURUGENZI MKUU

Karibu katika toleo la tatu la Jarida la Mtandaoni kutoka Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA). Katika jarida hili utasoma na kujifunza kuhusiana na kazi na huduma mbalimbali zinazofanywa na Mamlaka kama vile ujenzi wa mifumo inayoendana na mahitaji halisi ya Taasisi husika, utoaji wa huduma za ushauri na msaada wa kiufundi, uboreshaji wa njia za utoaji wa huduma za serikali mtandao, utengenezaji na uendeshaji wa mifumo na miundombinu ya **TEHAMA** Serikalini inayosaidia kuboresha ufanisi wa uendeshaji shughuli za utoaji wa huduma kwa Umma.

Hali kadhalika, katika Jarida hili utaweza kufahamu juhudi na shughuli mbalimbali zinazofanywa na Mamlaka katika utekelezaji wa dhana ya Serikali Mtandao.

Toleo hili ni muendelezo wa matoleo mengine yanayofuata yatakayokuhabarisha jitahada za e-GA katika kukuza na kuchochea matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) nchini, kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za umma na kuleta mabadiliko ya kijamii na kiuchumi.

Nichukue fursa hii kukukaribisha tena katika kurasa hizi ili upate kuifahamu vizuri e-GA na shughuli mbalimbali inazozitekeleza.

Nakutakia usomaji mwema

**Eng. Benedict Ndomba**
*Mkurugenzi Mkuu e-GA*



# Yaliyomo


Maagizo 12 ya Serikali katika kikao kazi cha Serikali Mtandao.....1

.Watumishi wa e-GA wahimizwa kuzingatia Misingi mikuu sita.....4

Wakaguzi wa ndani watakiwa kuzingatia Viwango na Miongozo.....5

Ndejembi aitaka e-GA kuendeleza Utafiti na Ubunifu.....6

e-GA yaweka Mikakati Madhubuti ya Kuijenga Serikali Kidijitali.....8

CHAVITA yaipongeza e-GA.....9

e-GA yakabidhi komputya 10 kwa jeshi la polisi.....10

Ndejembi azitaka Taasisi za Umma kushirikiana na e-GA.....11

Wakaguzi wa ndani wapewa mafunzo.....12

Karibuni.....13

Ahsanteni.....14

Kikao cha Wafanyakazi.....15

Kikao Kazi cha 3 cha Serikali Mtandao.....16

Michezo.....17

# MAELEKEZO 12 YA WAZIRI MHAGAMA KWA TAASISI ZA UMMA KUHUSU SERIKALI MTANDAO

Februari 08- 10 mwaka huu, Mamlaka ya Serikali Mta dao (e-GA) iliiandaa Kikao Kazi cha 3 cha Serikali Mtandao kilichofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Arusha (AICC).Kikao hicho, kiliwakutanisha wadau 1,624 wa Serikali Mtandao wa kada mbalimbali wakiwemo Wahasibu, Maafisa TEHAMA, Maafisa Masuuli, Maafisa Habari, Wahandisi n.k, kutoka katika Mashirika na Taasisi za Umma nchini ili kujadiliana na kuweka mikakati ya pamoja ya namna ya kuimarisha Serikali Mtandao katika Taasisi hizo.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Jenista Mhagama (Mb) akizungumza wakati wa Kikao kazi cha 3 cha Serikali Mtandao Februari 10, 2023

Ieleweke kuwa, Serikali Mtandao ni matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika utendaji kazi wa Taasisi za Umma na utoaji wa huduma kwa wananchi. Lengo la Serikali Mtandao ni kuongeza ufanisi wa utendaji kazi katika Taasisi za Umma pamoja na kuboresha utoaji wa huduma kwa umma ili huduma hizo zipatikane kwa urahisi, haraka na kwa gharama nafuu kupitia TEHAMA.

Hivyo basi, kuimarika kwa Serikali Mtandao kunatokana na utayari na ushiriki wa kada zote kwa kuwa kila mtumishi wa Serikali anayo nafasi ya kuhakikisha jitihada za Serikali Mtandao zinafanikiwa kupitia taaluma au fani yake na si suala la Maafisa TEHAMA pekee. Kwa muktadha huo, Mamlaka ya Serikali Mtandao iliona umuhimu wa kuwakutanisha watumishi wa umma wa kada mbalimbali katika kikao hicho ili kwa pamoja wajadili juu ya fursa, mafanikio, changamoto na kuweka mikakati mbalimbali ya namna ya kuimarisha jitihada za Serikali Mtandao nchini. Katika kikao hicho, jumla ya mada 22 zilizolenga kutathmini na kuimarisha nguzo kuu nne (4) za Serikali Mtandao ziliwasilishwa na wadau wa Serikali Mtandao kutoka katika Taasisi mbalimbali za Umma.

Mada hizo zilihusu namna ambavyo Taasisi hizo zimekuwa zikitekeleza jitihada za Serikali Mtandao kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA). Taasisi zilizowasilisha mada hizo ni pamoja na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ofisi ya Rais- TAMISEMI, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknlojia ya Habari, Wizara ya Fedha, Wizara ya Afya, Wizara ya Maji, Benki Kuu ya Tanzania (BOT), Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) na Mamlaka ya Usimamizi wa Ununuzi wa Umma (PPRA). Nyingine ni Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Wakala wa Ununuzi Serikalini (GPSA), Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL), Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), Tume ya TEHAMA (ICTC), Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA). Kupitia mada hizo, washiriki walipata nafasi ya kuuliza maswali na kupata majibu pamoja na ufafanuzi wa hoja walizowasilisha wakati wa majadiliano na hatimaye kuweka maazimio 12. Maazimio hayo yaliwasilishwa mbele ya Mhe. Jenista Mhagama (Mb) Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishiwa Umma na Utawala Bora (OR-MUUUB) na Bw. Priscus Kiwango Mkurugenzi wa TEHAMA Serikalini (OR-MUUUB).




Wadau wa Serikali Mtandao kutoka Taasisi mbalilmbali za Umma wakisikiliza kwa makini moja ya mada zilizotolewa wakati wa kikao kazi cha 3 cha Serikali Mtandao kilichofanyika Jijini Arusha kuanzia tarehe 8 - 10 Februari 2023.



Bw. Priscus Kiwango Mkurugenzi wa TEHAMA Serikalini akisoma maazimio ya Kikao Kazi cha 3 cha Serikali Mtandao mbele ya Mhe Waziri na wajumbe wengine waliohudhuria kikao hicho

Waziri Mhagama aliyapokea maazimio hayo na kuagiza kuwa ni maelekezo sahihi ya Serikali na kuwataka viongozi wote wa Taasisi za Umma, Maafisa TEHAMA pamoja na watumishi wote kuyatekeleza kuanzia Februari 10, mwaka huu.

Maelekezo hayo ni pamoja na; Taasisi za Umma kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika utoaji wa huduma kwa wananchi kwa njia ya kidijitali ili kuboresha utendaji kazi wa Taasisi za Umma, Taasisi za Umma zihakikishe zinaendesha shughuli za kawaida za Taasisi kama vile uendeshaji wa vikao vya menejimenti, vikao vya bodi, vikao vya halmashauri na vikao vya mabaraza ya madiwani kidijitali ili kupunguza matumizi ya karatasi.

Kuhuisha Tovuti za Taasisi ili kuendana na teknolojia ya kisasa na kuwa na taarifa sahihi na zinazoendana na wakati muda wote,Taasisi za umma zitoe kipaumbele katika masuala ya utafiti na ubunifu kwenye eneo la TEHAMA ili kuibua Mifumo ya TEHAMA itakayowezesha taifa kuendana na kasi ya maendeleo ya viwanda (4th Industrial Revolution), ikiwemo kutenga rasilimali fedha kwa ajili ya ubunifu.

“Mamlaka ya Serkali Mtandao (e-GA) kwa kushirikiana na Taasisi za Umma iendelee kujenga Mifumo shirikishi na Mifumo ya kisekta katika jitihada za kupunguza urudufu wa Mifumo ya TEHAMA katika utumishi wa umma.



Bw. Michael Moshiro Mkurugenzi wa TEHAMA kutoka PPRA akiwasilisha mada juu ya Mfumo mpya wa Manunuzi Serikalini (NeST) wakati wa kikao kazi cha 3 cha Serikali mtandao kilichofanyika Jijini Arusha Mwezi februari 2023.

“Kupitia kikao hiki, jumla ya mada 22 zinazohusu Serikali Mtandao zimewasilishwa na mmepata nafasi ya kufanya majadiliano kwa kina kwa muda wote wa siku tatu mlizokuwa hapa na kuweka maazimio 12 sasa mimi haya maazimio nimeyapokea na ninayatoa hapa kama maelekezo ya Serikali kwa Taasisi zote za umma kuanzia sasa”, alisema Mhagama.

Alisisitiza kuwa maazimio hayo yote ni muhimu katika ujenzi wa Serikali Mtandao kwakuwa yanalenga kuboresha namna Taasisi na Mashirika ya Umma yanavyoweza kutumia TEHAMA ili kuongeza ufanisi wa utendaji kazi katika Taasisi pamoja na kuboresha utoaji wa huduma kwa umma.

Naelekeza pia Wakuu wa Taasisi za Umma wajiunge kwenye Mfumo Mkuu wa Serikali wa kubadilishana taarifa (Government Enterprise Service Bus - GovESB) ili kuwezesha Mifumo kubadilishana taarifa”, alisisitiza Mhagama.

Ili kupunguza gharama na kuongeza usalama wa taarifa za serikali, Waziri Mhagama alizielekeza Taasisi za Umma kuhifadhi Mifumo yao kwenye vituo vya kuhifadhi data vya Serikali vilivyoidhinishwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) pamoja na kusisitiza kuendelea kuimarisha Usalama wa

Mifumo iliyokwishajengwa ikiwa ni pamoja na kuwa na Vituo vya Kujikinga na Majanga.

Aidha, Waziri Mhagama aliwataka Wakuu wa Taasisi za Umma wasimamie kikamilifu Utekelezaji wa Sheria ya Serikali Mtandao Na. 10 ya Mwaka 2019 na Kanuni zake za Mwaka 2020 hasa uanzishwaji wa Kamati ya Uongozi w TEHAMA (Institutional ICT Steering Committee) na kusimamia utendaji kazi wa kamati hizo.

"Ni muhimu kuwe na utaratibu wa kuwafanyia upekuzi pamoja na matamko ya kiapo kwa watumishi wa TEHAMA kwa kuwa wanasimamia Mifumo na data nyeti za Serikali lakini pia Serikali kwa kushirikiana na Sekta Binafsi tuweke mkakati wa kuwaandaa wanafunzi wa Vyuo vya elimu ya juu katika kufanya ubunifu katika masuala ya Serikali Mtandao na TEHAMA kwa ujumla"aliongeza Mhagama.

Maelekezo mengine yaliyotolewa ni pamoja na Serikali iwekeze katika kuanza kutengeneza vifaa vya TEHAMA hapa nchini na Mifumo ya TEHAMA ya Serikali inayojengwa iwe endelevu (sustainable) ili kuepuka kubadilisha Mifumo mara kwa mara kwa kuwa hadi Mfumo kuanza kutumika kunakuwa na uwekezaji mkubwa, ikiwemo mafunzo kwa watumiaji.

Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) huandaa Vikao Kazi vya Serikali Mtandao kwa kuzingatia mpango mkakati wa Mamlaka wa 2021/2022 – 2025/2026




Wadau wa Serikali Mtandao kutoka Taasisi mbalilmbali za Umma wakisikiliza kwa makini moja ya mada zilizotolewa wakati wa kikao kazi cha 3 cha Serikali Mtandao kilichofanyika Jijini Arusha kuanzia tarehe 8 - 10 Februari 2023.

# WATUMISHI WA e-GA WAHIMIZWA KUFANYA KAZI KWA KUZINGATIA MISINGI MIKUU SITA YA MAMLAKA



Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao Eng. Benedict Ndomba akizungumza na Watumishi wa Mamlaka wakati wa kikao cha watumishi Machi 16, 2023 Jijini Dar Es Salaam

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), Mhandisi Benedict Ndomba, amewataka watumishi wa Mamlaka hiyo kufanya kazi kwa kuzingatia misingi mikuu sita ya Taasisi.

Ndomba alisema hayo Machi 16, Mwaka huu wakati wa kikao cha Watumishi wa Mamlaka kilichofanyika kwa muda wa siku tatu katika ukumbi wa Karimjee jijini Dar es Salaam kwa lengo la kuwajengea uwezo watumishi hao katika masuala mbalimbali yanayohusu utumishi wa umma.

"e-GA inaongozwa na misingi mikuu sita ambayo inaelekeza kuhusu tabia na mwenendo wa watumishi wake kwa ngazi zote na kufafanua utamaduni wa mahali pa kazi ili kuhakikisha watumishi wote na wateja wa Mamlaka, wanao uelewa wa pamoja wa jinsi wanavyotakiwa kuhudumiwa na nini kichotarajiwa kutoka kwao", alisema Ndomba.

Aidha, Ndomba aliwakumbusha watumishi wote wa Mamlaka kuzingatia misingi hiyo ambayo ni uadilifu, ubunifu, kutathmini wateja, ushirikiano, kufanya kazi kwa pamoja na weledi katika utendaji kazi wao wa kila siku.

Alifafanua kuwa, Mamlaka imekuwa taasisi ya mfano inayofanya shughuli zake za kila siku kwa kasi na ari inayokubalika, kutokana na uadilifu mkubwa wa Menejimenti na watumishi waliodhamiria kuweka juhudi kubwa katika kuboresha utendaji wa Serikali na utoaji huduma bora kwa umma.

"Nawakumbusha watumishi wote kuimarisha uadilifu na kila mtumishi kutimiza wajibu wake kwa kufanya kazi kwa bidii, nidhamu na kwa weledi kwa kuzingatia misingi hiyo huku Mamlaka ikiendelea na jitihada mbalimbali za kuhakikisha kuwa watumishi wanafanya kazi katika mazingira bora na salama", alisisitiza Ndomba.

Katika kikao hicho mada mbalimbali zilizolenga kujenga uelewa na ufahamu kwa watumishi ziliwasilishwa ikiwemo Afya mahali pa kazi, Rushwa mahala pa kazi, Maadili ya utendaji, Haki na Wajibu, HIV/AIDS na magonjwa sugu yasiyoambukiza, mawasiliano mazuri kwa utendaji bora wa kazi, Namna ya kukabiliana na msongo wa mawazo na maisha kazini n.k

Aidha, Kikao hicho kilihitimishwa na Bonanza la Michezo lilifanyika katika viwanja vya gymkhana michezo mbalimbali ikiwemo kukimbiza kuku, kuvuta kamba, kutembea kwa kutumia magunia, kutembea na yai kwenye kijiko, mbio fupi n.k



Watumishi wa e-GA wakifuatilia mada mbalimbali wakati wa kikao kazi cha Watumishi.

# WAKAGUZI WA NDANI WATAKIWA KUZINGATIA VIWANGO NA MIONGOZO YA SERIKALI MTANDAO KATIKA MIRADI YA TEHAMA

Kaimu Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Hesabu za Serikali (IAG) Mwanyika Semroki, amewataka Wakaguzi wa Ndani kuhakikisha Mifumo ya TEHAMA inayoanzishwa katika Taasisi zao inazingatia miongozo na viwango vilivyowekwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA).

Mwanyika alitoa kauli hiyo Machi 10, Mwaka huu wakati akifunga mafunzo maalum ya ukaguzi wa Mifumo na Miradi ya TEHAMA yaliyotolewa kwa Wakaguzi wa Ndani wa halmashauri na Tawala za Mikoa yaliyofanyika kwa siku tano mkoani Morogoro.

"Mnapokwenda kutekeleza majukumu yenu katika Taasisi zenu, lazima muhoji kama Miradi na Mifumo ya TEHAMA pamoja na mahitaji ya mtumiaji (Taasisi) kama yanaendana na viwango na miongozo ya e-GA" alisema.

Mwanyika aliongeza kuwa, Mifumo ya TEHAMA inapaswa kuwa rahisi na rafiki kwa mtumiaji hivyo, kama Mifumo inayotengenezwa katika Taasisi za Umma si rahisi na rafiki kwa watumiaji basi haifai na hivyo inapaswa kuboreshwa.
Aidha, Mwanyika alifafanua kuwa, mafunzo hayo ni muhimu kwa kuwa yatawawezesha Wakaguzi wa Ndani kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na kuisaidia Serikali kuona thamani halisi ya fedha ilizowekeza katika Miradi na Mifumo ya TEHAMA.

Akitoa ufafanuzi kuhusu maoni yaliyotolewa na washiriki wa mafunzo hayo, Mwanyika alisema kuwa, mafunzo hayo yatakuwa endelevu ili kuhakikisha Wakaguzi wa Ndani katika halmashauri na Tawala za mikoa yote wanapatiwa mafunzo hayo.

Kwa upande wake Meneja Udhibiti na Viwango vya Serikali Mtandao Bi. Sultana Seif Alisema kuwa, e-GA kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Hesabu za Serikali itahakikisha kuwa Wakaguzi wote wa Nadani katika halmashauri na Tawala za Mikoa wanapata mafunzo hayo kabla ya kuisha mwaka wa fedha 2022/2023.

"Kabla ya mwaka huu wa fedha kuisha, tutahakikisha Wakaguzi wote wa Ndani tunawajengea uwezo wa kukagua Mifumo na Miradi ya TEHAMA ili kuweza kuibua hoja za ukaguzi mapema na kufanyiwa kazi kabla ya Mkaguzi wa nje", alisema Bi. Sultana.

Akitoa salamu za shukran kwa niaba ya washiriki Mwidikila Lawrence Silanda - Mkaguzi Mķuu wa Ndani Halmashauri ya Sengerema alisema kuwa, Mafunzo hayo yamewasaidia kufahamu namna ya kufanya ukaguzi katika Mifumo na Miradi ya TEHAMA na kupendekeza mafunzo hayo yawe endelevu kulingana na mabadiliko ya teknolojia yanayoibuka mara kwa mara.





Kaimu Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Hesabu za Serikali (IAG) Mwanyika Semroki akizungumza na wakaguzi wa Ndani kutoka Halmashauri na Tawala za Mikoa Nchini wakati wa mafunzo maalum ya ukaguzi wa Mifumo na Miradi ya TEHAMA yaliyofanyika kwa siku tano mkoani Morogoro.

# Ndejembi aitaka e-GA kuendeleza utafiti na ubunifu wa Mifumo ya TEHAMA



Naibu Waziri Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Deogratius Ndejembi akizungumza wakati wa ufunguzi wa kikao kazi cha 3 cha Serikali Mtandao kilichofanyika Mwezi Februari Jijini Arusha

Naibu Waziri Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Deogratius Ndejembi (Mb), ameitaka Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kuendelea kufanya utafiti na ubunifu wa Mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ili kuibua Mifumo itakayosaidia kuimarisha sekta ya viwanda, biashara na uwekezaji ili kuleta maendeleo kwa taifa.

Mhe. Ndejembi ametoa wito huo Februari 8, Mwaka huu wakati akifungua kikao kazi cha tatu cha Serikali Mtandao kilichofanyika hivi karibuni katika Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Arusha (AICC) jijini Arusha.

Ili kuhakikisha matumizi sahihi na salama ya TEHAMA katika Taasisi za Umma, Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) haina budi kufanya tafiti zitakazowezesha ubunifu wa Mifumo itakayoboresha utendaji kazi katika Taasisi za Umma na hivyo kuchochea utoaji wa huduma bora kwa wananchi", alisisitiza Mhe. Ndejembi.

Aidha, Mhe. Ndejembi alisema kuwa, Serikali ya awamu ya sita imetoa kipaumbele kwenye matumizi ya TEHAMA hususani katika masuala ya utafiti na ubunifu kwenye eneo la TEHAMA ili kuimairisha uchumi wa kidigitali katika sekta ya viwanda na biashara.

Kwa upande wake Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Dkt. Laurean Ndumbaro, alisema kuwa utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao ni moja ya maeneo muhimu ya maboresho yaliyofanyika na yanayoendelea kufanywa katika Utumishi wa Umma ambayo yamesaidia kuboresha utendaji kazi na utoaji wa huduma kwa Umma.

Dkt. Ndumbaro alisema kuwa, Serikali imeweka mazingira mazuri ya kisera, kisheria, na kiusimamizi ili kuhakikisha matumizi sahihi na salama ya TEHAMA katika Taasisi za Umma na yanayoleta tija na ufanisi unaoboresha utendaji kazi wa Taasisi hizo na kuwaondolea wananchi kero mbalimbali.

> Serikali kupitia Ofisi ya Rais Menejimenti ya Umma na Utawala Bora, itaendelea kuhakikisha inaweka mazingira wezeshi ya kisera na kisheria pamoja na kuijengea uwezo Mamlaka ya Serikali Mtandao ili iweze kufikia malengo iliyojiwekea

"Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora inaunga mkono juhudi za Serikali za kuleta mageuzi katika utoaji wa huduma za Serikali kidijiti ili kupanua wigo wa upatikanaji wa huduma mtandao kwa umma" alisema Dkt. Ndumbaro.



Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Dkt. Laurean Ndumbaro akizungumza katika kikao kazi cha 3 cha Serikali Mtandao kilichofanyika Mwezi Februari Jijini Arusha

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Eng. Benedict Ndomba alisema, katika kipindi cha miaka 10 tangu kuanzishwa kwake, e-GA imefanikiwa kuyatimizia malengo mbalimbali iliyojipangia kwa ufanisi mkubwa kutokana na uzingatiaji wa Misingi Mikuu sita (6) inayoongoza utendaji kazi ndani ya Mamlaka, ambayo ni weledi, ubunifu, ushirikiano, kuthamini wateja, uadilifu, na kufanya kazi kwa pamoja.

Eng. Ndomba alisema kuwa, ushirikiano na utendaji kazi mzuri na wadau wa Serikali Mtandao umeisadia Mamlaka kufika malengo yake ya kuhakikisha kuwa matumizi ya TEHAMA katika Taasisi za umma yanakuwa na tija na ufanisi ili kurahisiaha upatikanaji wa huduma kwa wananchi kwa urahisi na haraka pamoja na kuhoresha




Wadau wa Serikali Mtandao kutoka Taasisi mbalilmbali za Umma wakisikiliza kwa makini moja ya mada zilizotolewa wakati wa kikao kazi cha 3 cha Serikali Mtandao kilichofanyika Jijini Arusha kuanzia tarehe 8 - 10 Februari 2023.

huduma hizo.

"Mamlaka kwa kushirikiana na Taasisi mbalimbali za Umma imefanikiwa kusanifu, kujenga na kusimamia uendeshaji wa Mifumo na Miundombinu mbalimbali ya Serikali Mtandao katika Taasisi za Umma ili kuboresha utendaji kazi na utoaji wa huduma mpya za Serikali Mtandao kwa Umma", alisema Eng. Ndomba.

Aidha, Ndomba alizitaja baadhi ya changamoto zinazoikabili Mamlaka katika uendeshaji na usimamizi wa Mifumo kuwa ni pamoja na; baadhi ya Taasisi kuwa na Mifumo isiyobadilishana taarifa, Mifumo isiyowasiliana na Mifumo mingine pamoja na upungufu wa nyenzo muhimu za kukabiliana na matishio ya usalama wa mtandaoni yanayoongezeka kutokana na kasi ya ukuaji wa teknolojia.

Kikao Kazi cha 3 cha Serikali Mtandao, kilifanyika Februari 8 hadi 10 mwaka huu katika ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Arusha (AICC) na kuwakutanisha wadau 1624 wa Serikali Mtandao kutoka katika Mashirika na Taasisi za Umma, kwa lengo la kuweka mikakati mbalimbali ya kukuza Serikali Mtandao nchini wakiongozwa na kauli mbiu isemayo "Mifumo Jumuishi ya TEHAMA kwa Utoaji wa Huduma Bora kwa Umma.

# e-GA yaweka Mikakati Madhubuti ya Kuijenga Serikali Kidijitali

Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) itaendele imeweka mikakati madhubuti ya utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao itakayosaidia kuimarisha na kuijenga serikali kidijitali.

Kauli hiyo ilitolewa Februari 23, Mwaka huu jijini Dodoma na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), Mhandisi Benedict Ndomba wakati alipofanya mkutano na waandishi wa habari, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka.

"Katika kipindi cha miaka 10 ijayo, e-GA itaandaa na kutekeleza mikakati itakayojiwekea ili kuimarisha zaidi utekelezaji wa jitihada za Serikali kimtandao na kuhahikisha kuwa Taasisi za Umma zinatoa huduma kwa wananchi kwa njia ya kidijitali", alisema Ndomba..




Aidha, Ndomba alifafanua kuwa, utekelezaji wa mikakati hiyo utasaidia uwepo wa sehemu moja ambayo huduma zote za mtandao zitakuwa zinapatikana, pamoja na kuwa na uwezo wa kutumia teknolojia mpya zinazoibuka, hasa zile za akili bandia, sarafu za kidijiti na teknolojia za kifedha, ili kuwezesha maboresho ya kiutendaji katika Taasisi za Umma na utoaji wa huduma kwa Umma.

Ndomba aliongeza kuwa, kupitia utekelezaji wa mikakati hiyo Mamlaka itahakikisha kuwa, idadi ya vijana wa kitanzania wenye uwezo mkubwa wa ubunifu katika utekelezaji wa jitihada za Serikali mtandao inaongezeka pamoja na uwepo wa Mifumo na Miundombinu ya Serikali mtandao iliyo bora na imara zaidi.

"Ili kufikia yote haya katika kipindi kijacho, Mamlaka itaendela kuunganisha Mifumo ya Taasisi za Umma kwenye Mfumo wa Serikali wa kubadilishana Taarifa ***(Government Enterprise Service Bus - GovESB)*** na kuendeleza shughuli za tafiti na ubunifu katika matumizi ya teknolojia mpya za TEHAMA ili kuibua huduma mpya kwa umma na kuwezesha matumizi sahihi ya teknolojia", alisema Ndomba.

Katika kuimarisha Serikali Mtandao nchini, Mamlaka itaendelea kupitia na kutathmini hali ya usalama wa Mifumo na Miundombinu ya Serikali Mtandao na kuzishauri Taasisi za Umma katika maeneo ya kuboresha, pamoja na kufuatilia utekelezaji wake ili kuhakikisha kuwa Mifumo na Miundombinu ya TEHAMA inafanya kazi wakati wote kwa ufanisi na usalama", alisisitiza Ndomba.

Aidha, Ndomba alisema kuwa, Mamlaka imejipanga na itaendelea kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kusimamia uzingatiaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao kwa Taasisi za Umma ili kujenga Serikali ya Kidijitali.



# CHAVITA yaipongeza eGA kwa huduma za Serikali Mtandao jumuishi kwa watu wenye ulemavu

Mwenyekiti wa Chama cha Viziwi Tanzania (CHAVITA) Wilaya ya Rufiji Mkoa wa Pwani Bw. Suleiman Zalala ameipongeza Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kwa huduma jumuishi za Utekelezaji wa Jitihada za Serikali Mtandao kwa watu wenye ulemavu

Mwenyekiti ametoa pongezi hizo Februari 9, Mwaka huu wakati wa kilele cha kikao kazi cha tatu (3) cha Serikali Mtandao kilichofanyika hivi karibuni katika Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Arusha (AICC) jijini Arusha.

Bw. Zalala ameishukuru Mamlaka kwa kuthamini na kuona mchango wa kundi maalumu la watu wenye uelemavu kushiriki katika mafunzo hayo ili kuboresha huduma jumuishi za Serikali Mtandao kwa watu wenye walemavu.

Mwenyekiti amesema CHAVITA imekuwa na ushirikiano wa muda mrefu na eGA katika programu mbalimbali za mafunzo zinazoandaliwa na Mamlaka kwa watu wenye ulemavu na kwamba mafunzo hayo yamekuwa yakiwajengea uwezo na uelewa mkubwa wa utekelezaji wa jitahada za Serikali Mtandao katika utoaji wa huduma mbalimbali kwa wananchi.

“Tumepata kujifunza na kupata uelewa juu ya mabadiliko mbalimbali ya teknolojia katika utoaji wa huduma na huduma mbalimbali zinazowezeshwa na eGA kwa wananchi kama vile ununuzi wa Luku, bill za maji n.k”

Aidha, Mwenyekiti ameomba mafunzo hayo yawe chachu kwa Taasisi nyingine za Umma kuiga mfano wa kile kilichofanywa na Mamlaka kwa kuwashirikisha makundi maalum kwenye uandaaji wa mafunzo na programu mbalimbali zinazotekelezwa na taasisi zao .

Nae Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Eng. Benedict Ndomba amewashukuru wadau wote waliohudhuria kikao kazi hicho na kwa michango yao itakayosaidia kufanikisha na kuimarisha utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao kwa ajili ya kuboresha utendaji kazi wa Taasisi za umma, pamoja na utoaji wa huduma kwa umma.


“Naimani kuwa, kikao hiki kimewajengea uwezo zaidi washiriki wote kuhusu Serikali Mtandao na kila mdau ametambua namna ambavyo anaweza kufanikisha jitihada za Serikali Mtandao kupitia sekta yake” Alisema Eng. Ndomba

Eng. Ndomba aliongeza kuwa washiriki 1624 wamehudhuria kikao hicho na mada 22 ziliwasilishwa na wadau kutoka katika taasisi mbalimbali za Umma zilizolenga kutathmini na kuimarisha nguzo kuu Nne (4) za Serikali Mtandao.

Mkurugenzi amesema katika kikao hicho wadau wamepata fursa ya kujadili masuala mbalimbali ya ushirikiano katika kutekeleza jitihada za Serikali Mtandao nchini pamoja na kutafuta ufumbuzi wa changamoto za serikali mtandao zilizopo nchini ili kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii .

Vilevile washiriki wametoa maoni mbalimbali ya namna ya kukuza jitihada za Serikali Mtandao ikiwa ni pamoja na kushauri uboreshaji wa Mifumo mbalimbali inayotoa huduma kwa umma pamoja na kupanua wigo wa utoaji wa huduma za Serikali Mtandao katika maeneo mbalimbali nchini.

Mkurugenzi amesema Menejimenti ya Mamlaka imeyapokea maoni na ushauri uliotolewa na kwamba eGA ipo tayari kufanyia kazi maoni hayo yanayolenga kuboresha na kukuza jitihada za Serikali Mtandao nchini.



Mwenyekiti wa Chama cha Viziwi Tanzaia (CHAVITA ) katikati akiwa katika picha ya pamoja na Mkurugenzi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Eng. Benedict Ndomba kulia kwake pamoja na viongozi wengine wa Menejimenti ya e-GA na CHAVITA.

# e-GA YAKABIDHI KOMPYUTA 10 KWA JESHI LA POLISI

Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) imetoa mchango wa kompyuta 10 kwa Jeshi la Polisi nchini, ikiwa ni sehemu ya kuhamasisha matumizi ya teknolojia katika utoaji wa haki kwa wananchi.

Makabidhiano hayo yalifanyika Machi 13, Mwaka huu katika Ofisi za Mamlaka jijini Dar es Salaam ambapo kwa upande wa e-GA Bw. Benjamin Dotto Mkurugenzi wa Miundombinu na Uwezeshaji wa TEHAMA alikabidhi komputa hizo kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu Mhandisi. Benedict Ndomba.

Akiongea wakati wa makabidhiano hayo, Bw. Dotto alisema kuwa, e-GA imekuwa ikishirikiana na Taasisi mbalimbali za Umma likiwemo Jeshi la Polisi, katika kuhakikisha matumizi ya Teknolojia yanarahisisha utendaji kazi wa Taasisi na utoaji wa huduma kwa umma.

"Teknolojia hurahisisha mchakato wa utoaji wa haki na sisi e-GA tukaona ni vizuri kuchangia kwa kutoa kompyuta hizi ili zirahisishe mchakato wa haki jinai katika Jeshi la Polisi", alisema Dotto.
Kwa upande wake, Mkuu wa TEHAMA wa Jeshi la Polisi Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP) Justus Mafuru alisema kuwa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan, aliagiza kutengeneza Mfumo wa haki jinai ambao tayari umekwishatengenezwa.

"Kwa niaba ya IGP tunaishukuru e-GAkwa mchango huu wa kompyuta ambao utasaidia upatikanaji wa haki kwa wananchi kwa urahisi na haraka kupitia Teknolojia na kwakuwa Mfumo wa hakijinai umekwishatengenezwa kwa sasa tunahitaji vifaa", alisema ACP Mafuru.

Mamlaka ya Serikali Mtandao ni Taasisi ya Umma iliyoanzishwa kwa Sheria ya Serikali Mtandao Na. 10 ya mwaka 2019, ikiwa na majukumu ya kuratibu, kusimamia na kukuza jitihada za Serikali Mtandao, pamoja na kusimamia uzingatiaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao katika taasisi za umma.




Mkurugenzi wa Huduma na Uendeshaji wa Mamlaka ya Serikali Mtandao Bw. Benjamin Dotto akimkabidhi Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP) Justus Mafuru Kompyuta 10 zilizotolewa na Mamlaka ya Serikali Mtandao kwa Jeshi la Polisi kuhakikisha matumizi ya Teknolojia yanarahisisha utendaji kazi wa Taasisi na utoaji wa huduma kwa umma



# MHE. NDEJEMBI AZITAKA TAASISI ZA UMMA KUSHIRIKIANA NA e-GA

Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Deogratius Ndejembi (Mb) amezitaka Taasisi za Umma kushirikiana na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) katika kutengeneza Mifumo ya TEHAMA itakayorahisisha utoaji wa huduma bora kwa Wananchi.

Ndejembi alisema hayo Februari 17, Mwaka huu wakati alipofanya ziara ya kikazi ya siku moja kukagua utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya Mamlaka, katika Ofisi za e-GA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini zilizopo mkoani Iringa.

Aidha, Ndejembi aliipongeza e-GA kutokana na umahiri wake katika utendaji kazi ikiwemo uwezo wa kubuni, kusanifu na kujenga Mifumo mbalimbali ya TEHAMA ambayo imesaidia kuimarisha utendaji kazi wa Taasisi za Umma pamoja na kuboresha utoaji wa huduma bora kwa wananchi.

"Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuwa akisisitiza kujenga taifa la kidijitali kwa kuhakikisha huduma zote za Kiserikali zinatolewa kwa njia ya kidijitali, na kuwafikia wananchi wote kwa urahisi na haraka", alisema Ndejembi na kuongeza kuwa;

"Hata hivyo kuna baadhi ya taasisi za umma zimekuwa na ugumu wa kubadilika kuendana na kasi ya Rais, zinataka kujifanyia mambo kienyeji, natoa wito kwa taasisi hizo kuitumia e-GA katika kujenga Mifumo itakayosaidia upatikanaji wa huduma kwa wananchi kwa haraka".

Ndejembi alizitaja baadhi ya kazi zilizofanywa na e-GA kwa kushirikiana na taasisi nyingine za umma ambazo zimeleta matokeo chanya kwa taifa kuwa ni pamoja na utengenezaji wa Mfumo wa Malipo ya Serikali Kieletroniki (GePG) ambao umesaidia Serikali kufahamu mapato yanayoingia kila siku kwakuwa malipo yote kwa sasa hufanyika kupitia Mfumo huo.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Mhandisi Benedict Ndomba, alisema kuwa e-GA ipo tayari kushirikiana na Taasisi zote za umma katika ujenzi na usamimizi wa Mifumo ya TEHAMA ambayo itasaidia kuboresha utendaji kazi katika Taasisi hizo na utoaji wa hudumma kwa wananchi.

"Tutaendelea kushirikiana na Taasisi za Umma ili kuhakikisha huduma kwa wananchi zinatolewa kwa urahisi, haraka na gharama nafuu pamoja na kuboresha ufanisi na utendaji kazi katika Taasisi hizo", alisema Ndomba.



> "Baadhi ya maeneo jiografia yake ni ngumu kutoka eneo la makazi au Kijiji kimoja hadi zilipo ofisi za Halmashauri, na hivyo kuwa changamoto kwa wakazi wa maeneo hayo kupata huduma za serikali kwa urahisi Zaidi, hivyo ni vizuri e-GA ikajenga mifumo itakayorahisisha wakazi wa maeneo yenye changamoto kama hizi kupata huduma mahali walipo pasi na kufika ofisini"

# WAKAGUZI WA NDANI WA HALMASHAURI WAPEWA MAFUNZO YA UKAGUZI WA MIFUMO YA TEHAMA

Mamlaka ya Serikali Mtandao e-GA imewataka Wakaguzi wa ndani wa Halmashauri na Tawala za Mikoa kuzingatia sheria na miongozo ya Serikali Mtandao, wakati wa ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA katika Taasisi zao ili kupunguza hoja za ukaguzi.

Kauli hiyo imetolewa na Mkurugenzi Mkuu wa e-GA Mhandisi. Benedict Ndomba, wakati wa Mafunzo ya siku tano (05) ya kuwajengea uwezo Wakaguzi wa Ndani wa halmashauri na Tawala za Mikoa ili waweze kukagua Mifumo ya TEHAMA inayotumika katika Taasisi zao.

Ndomba alieleza kuwa, mafunzo hayo ni utekelezaji wa moja ya mapendekezo yaliyotolewa na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG) ya kuitaka e-GA kushirikiana na Taasisi za Umma kuandaa mpango mkakati na utekelezaji wake katika kushughulikia ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA.



"Mafunzo haya tumeyandaa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali (IAG) ili kuwawezesha Wakaguzi wa Ndani wa halmashauri na Tawala za Mikoa, kufanya ufuatiliaji wa miradi ya TEHAMA katika Taasisi zenu", alisema Ndomba.

Aidha, Ndomba aliwataka Wakaguzi wa Ndani kufanya kazi kwa karibu na e-GA na kuwasilisha changamoto zozote watakazokutana nazo wakati wa utekelezaji wa majukumu yao katika ukaguzi wa miradi ya TEHAMA na kuahidi kuzifanyia kazi kwa wakati.

Ndomba aliongeza kuwa, kupitia mafunzo hayo, wataalamu hao wataweza kubaini mapungufu yanayojitokeza katika miradi na mifumo ya TEHAMA katika taasisi zao na kuweza kushauri namna ya kuboresha.

Ndomba aliahidi kuwa, Mamlaka ya Serikali Mtandao itaendelea kuwajengea uwezo wataalamu hao kutokana na mabadiliko ya Teknolojia yanayoibuka kila mara.

Kwa upande wake mwakilishi wa washiriki wa mafunzo hayo Adeline Komba, alishukuru e-GA na Ofisi ya IAG kwa kufanikisha mafunzo hayo, kwani Wakaguzi wa Ndani wamekuwa wakiyahitaji mafunzo hayo kwa muda mrefu.

"Uelewa wa Wakaguzi wa Ndani si mkubwa na wamekuwa wa mwisho kupewa mafunzo hayo hivyo nashauri wapewe mafunzo mapema wakati wa ujenzi wa Mifumo", alisema Komba.

Vilevile Komba aliishauri e-GA kuwa na dawati maalum la kushughulikia changamoto mbalimbalimbali zinazojitokeza ili ziweze kutatuliwa kwa wakati, ushauri ambao ulipokelewa na

> "Sio vizuri kuwa na hoja za kiukaguzi hasa zile ambazo zinaweza kupatiwa suluhu kama vile, hoja ya kutokuwepo kwa sera ya TEHAMA katika Taasisi kwakuwa tayari miongozo imekwishaandaliwa na e-GA, hivyo kupitia mafunzo haya mtaweza kubaini namna gani mnaweza kuondokana na hoja za aina hiyo", alisisitiza Ndomba.

Mkurugenzi Mkuu wa e-GA, Mhandisi Benedict Ndomba na kuahidi kutekelezwa kupitia dawati la msaada 'helpdesk'.

Mafunzo hayo yamewakutanisha jumla ya washiriki 133 kutoka katika halmashauri na Tawala za Mikoa (13).

# KARIBUNI

Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) inawapongeza kwa kuteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kuiongoza Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (ORMUUUB)

Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), inaahidi kutoa ushirikiano wa dhati kwa viongozi wote na ipo tayari kupokea ushauri wenu ili kuimarisha ujenzi wa Serikali ya Kigijitali, unaolenga kuimarisha utendaji kazi katika Taasisi na kuboresha utoaji wa huduma bora kwa wananchi. Tunafurahi kufanya kazi pamoja na karibuni sana tuijenge Serikali ya Kidijitali pamoja.



**Mhe. George B. M. Simbachawene**
WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (ORMUUUB)



**Mhe. Ridhiwan J. Kikwete**
Naibu Waziri - ORMUUUB



**Bw. Juma S. Mkomi**
Katibu Mkuu - ORMUUUB

# AHSANTENI

Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), inawashukuru kwa uongozi mahiri na ushirikiano mlioutoa wakati wote mlipokuwa viongozi katika Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (ORMUUUB)

Mamlaka inatambua na kuthamini michango mliyotoa katika ujenzi wa Serikali ya Kidijitali. Aidha, Mamlaka itaendelea kuyaenzi mambo yote mazuri mliyotuachia.Tunajivunia sana kufanya kazi pamoja, tunawatakia heri katika majukumu yenu mapya. Asanteni, tumeweza kuijenga Serikali ya Kidijitali pamoja na kwaherini.



**Mhe. Jenista J. Mhagama**
Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (Bunge, Sera na Uratibu)



**Mhe. Deogratius Ndejembi**
Naibu Waziri - TAMISEMI



**Dkt. Laurean Ndumbaro**
Aliyekuwa Katibu Mkuu - ORMUUUB

# KIKAO CHA WAFANYAKAZI



Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao Eng. Benedict Ndomba akizungumza na Watumishi wa Mamlaka wakati wa kikao cha watumishi Machi 16, 2023 Jijini Dar Es Salaam



Dkt. Mauki akitoa Mada kwa watumishi wa e-GA wakati wa kikao kazi cha watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao tarehe 17 Machi 2023 jijini Dar Es Salaam



Mwakilishi kutoka Wakala wa Usalama na Afya mahali pa kazi (OSHA) akitoa Mada ya Usalama mahala pa kazi kwa watumishi wa e-GA wakati wa kikao kazi cha watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao tarehe 17 Machi 2023 jijini Dar Es Salaam



Mwakilishi kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora akitoa Mada kwa watumishi wa e-GA wakati wa kikao kazi cha watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao tarehe 17 Machi 2023 jijini Dar Es Salaam



Mkurugenzi wa Huduma na Uendeshaji wa Mamlaka ya Serikali Mtandao Bw. Benjamin Dotto akisikiliza moja ya Mada zilizotolewa wakati wa kikao kazi cha watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao



Watumishi wa e-GA wakisikiliza kwa makini mada zilizowasilishwa wakati wa Kikao cha Wafanyakazi



Mwakilishi kutoka Taasisi ya kuzuia na kupambana na Rushwa (TAKUKURU) akitoa Mada ya Rushwa kwa watumishi wa e-GA wakati wa kikao kazi cha watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao



Bw. Mosses akitoa Mada kwa watumishi wa e-GA wakati wa kikao kazi cha watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao tarehe 17 Machi 2023 jijini Dar Es Salaam

# KIKAO KAZI CHA SERIKALI MTANDAO



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Jenista J Mhagama akizungumza katika kikao kazi cha 3 cha serikali mtandao wakati akifunga kikao kazi hicho jijini Arusha tarehe 10 Februari 2023



Naibu Waziri Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Deogratius Ndejembi akizungumza wakati wa ufunguzi wa kikao kazi cha 3 cha Serikali Mtandao kilichofanyika Mwezi Februari Jijini Arusha



Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) Mhandisi Benedict Ndomba akieleza Mafanikio ya Mamlaka ndani ya miaka 10 wakati wa kikao kazi cha 3 cha Serikali mtandao kilichofanyika Jijini Arusha Kuanzia tarehe 8 - 10 Februari 2023



Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma Bw. Xavier Daudi akitoa neno la utangulizi kabla ya kumkaribisha Waziri Mhe. Jenista Mhagama kufunga kikao kazi cha 3 cha serikali mtandao jijini Arusha tarehe 10 Februari 2023.



Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Dkt. Laurean Ndumbaro akitoa neno la utangulizi kabla ya kumkaribisha Naibu Waziri Mhe. Deogratius Ndejembi kufungua kikao kazi cha 3 cha serikali mtandao jijini Arusha.




Wadau wa Serikali Mtandao kutoka Taasisi mbalilmbali za Umma wakisikiliza kwa makini moja ya mada zilizotolewa wakati wa kikao kazi cha 3 cha Serikali Mtandao kilichofanyika Jijini Arusha kuanzia tarehe 8 - 10 Februari 2023.




Wadau wa Serikali Mtandao kutoka Taasisi mbalilmbali za Umma wakisikiliza kwa makini moja ya mada zilizotolewa wakati wa kikao kazi cha 3 cha Serikali Mtandao kilichofanyika Jijini Arusha kuanzia tarehe 8 - 10 Februari 2023.




Bw. Michael Moshiro Mkurugenzi wa TEHAMA kutoka PPRA akiwasilisha mada juu ya Mfumo mpya wa Manunuzi Serikalini (NeST) wakati wa kikao kazi cha 3 cha Serikali mtandao kilichofanyika Jijini Arusha Mwezi februari 2023.

# MICHEZO



Wachezaji wa Mpira wa Miguu kutoka Kurugenzi ya Huduma na Uwezeshaji - (DCS) wakiwa katika picha ya pamoja



Wachezaji wa Mpira wa Miguu kutoka kurugenzi ya Udhibiti wa Viwango, Miongozo na Usalama wa TEHAMA (DCSM) wakiwa katika picha ya pamoja



Timu kutoka Kurugenzi ya Huduma na Uwezeshaji - (DCS) ikikabidhiwa kombe mara baada ya kushinda kwa kuongoza Ligi kwa jumla ya pointi kumi (10).



Watumishi kutoka Kurugenzi ya Huduma na Uwezeshaji - (DCS) wakivuta kamba na kuibuka washindi



Khadija Mzenzi akipokea zawadi baada ya kuibuka mshindi wa pili mbio za mita 100



Wachezaji wa Mpira wa Miguu wakiwa katika harakati ya kugombania mpira wakati wa mashindano yaliyojumuisha timu kutoka Kurugenzi mbalimbali za Mamlaka ya Serikali Mtandao



Sultana Seif akipokea zawadi baada ya kuibuka mshindi wa kwanza mbio za mita 100



Watumishi kutoka Kurugenzi ya Huduma na Uwezeshaji - (DCS) ikishangilia kombe la ushindi

**Jarida hili limeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano cha Mamlaka ya Serikali Mtandao kikiongozwa na bodi ya wahariri.**

Mwenyekiti : *Eng. Benedict Ndomba*

Mhariri : *Subira Kaswaga*

Mhariri Msaidizi : *Rainer Budodi*

Waandishi : *Queenter Mawinda*
*Catherine Peter*

Msanifu wa picha : *Edger Msamba*

Mpiga picha : *Mussa Enock*

*"Karibu tujenge Serikali kidijitali"*

**Mamlaka ya Serikali Mtandao**
**S.L.P 2833 Dodoma,**
**Mtaa wa Mtandao,**
**MTUMBA**
Tovuti: www.ega.go.tz
Barua pepe: info@ega.go.tz